## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# MAELEZO YA UTANGULIZI YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) KATIKA PROGRAMU YA MAGEUZI YA KUKIJANISHA TANZANIA

**DODOMA** **04 JUNI, 2026**

***Mheshimiwa, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi,*** *Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

***Mheshimiwa, Mussa Azzan Zungu****, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

***Dkt. Asha Rose Migiro,*** *Katibu Mkuu wa CCM Taifa;*

***Mheshimiwa, Hamza Hassan Juma****, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi-Zanzibar;*

***Washeshimiwa Mawaziri*** *mliopo hapa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;*

***Mheshimiwa,*** **Rosemary Sitaki** ***Senyamule,*** *Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;*

***Waheshimiwa Wakuu wa mikoa*** *mliopo hapa;*

***Manaibu Waziri*** *mliopo hapa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;*

***Mheshimiwa, Jackson Kiswaga****, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira;*

***Mheshimiwa, Dkt. Damas Ndumbaro****, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria;*

***Waheshimiwa Wabunge;***

***Mheshimiwa Dkt. Richard S. Muyungi****, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira);*

***Ndugu Makatibu Wakuu*** *kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;*

***Naibu Makatibu Wakuu*** *kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;*

***Bi. Clara Makenya****, Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa Nchini Tanzania (UNEP);*

***Ndugu Makatibu Tawala*** *wa Mikoa yote Tanzania Bara;*

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***

***Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri zote Nchini;***

***Viongozi wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi,*** *kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar*

***Viongozi wa vyama vya Siasa;***

***Waheshimiwa Madiwani;***

***Viongozi na Maafisa wa Serikali mliopo hapa,*** *kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar*

***Ndugu Wanahabari;***

***Ndugu Wananchi;***

***Kazi na Utu……!***
***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema kushiriki kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Mazingira Duniani.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani hapa Dodoma. Tumefarijika sana kupata heshima kubwa ya kuwa na wewe hapa siku ya leo pamoja na majukumu mengi ya Kitaifa uliyonayo. Hakika, uwepo wako hapa ni uthibitisho tosha kuwa wewe ni mwana mazingira mahiri. Mafanikio makubwa kitaifa na kimataifa ambayo nchi yetu imeyapata yanatokana na uongozi wako adili na maono yako.

Lakini zaidi sana napenda kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kazi nzuri unayoendelea kuifanya katika kuliongoza Taifa letu kwa hekima, busara na weledi mkubwa. Sisi unaotuongoza tunatambua majukumu makubwa uliyonayo na tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kukujalia afya na siha njema katika utekelezaji wa majukumu yako.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Leo, Watanzania tunaungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani ambayo hufanyika tarehe 5 Juni ya kila mwaka. Historia ya maadhimisho haya, yanatokana na maamuzi ya Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa kwamba, kuwe na siku maalum ya maadhimisho ya mazingira duniani kote, ikiwa ni kumbukumbu ya mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira uliofanyika mwaka 1972 mjini Stockholm, Sweden. Kutokana na umuhimu wa malengo ya maazimio hayo, mataifa mbalimbali yanayotambua umuhimu wa hifadhi ya mazingira, Tanzania ikiwa miongoni mwao yamekuwa yakiendeleza utamaduni wa

kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka ifikapo tarehe kama ya leo na huadhimishwa kwa ujumbe maalum unaotolewa na Umoja wa Mataifa.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kimataifa kwa mwaka huu 2026 yatafanyika **Baku** nchini **Azerbaijan** na kaulimbiu itakayoongoza maadhimisho haya Kimataifa, ***"Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi".*** Kaulimbiu hii inasisitiza umuhimu wa kuongeza kasi na juhudi za kupunguza uzalishaji wa gesijoto, kukuza matumizi ya nishati mbadala, na kuimarisha uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, kaulimbiu hii pia inahimiza Jumuiya ya Kimataifa kuchukua hatua za ziada na haraka za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimeendelea kujidhihirisha kupitia ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko, upungufu wa maji, kuibuka kwa magonjwa pamoja na kutishia usalama wa chakula duniani.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Kama ilivyo utamaduni wetu umejiwekea utaratibu wa kuwa na kaulimbiu ya kitaifa ambayo inaakisi vipaumbele vya Uhifadhi wa Mazingira pamoja na changamoto zilizopo ili kuendeleza juhudi za kukabiliana nazo. Hivyo kwa mwaka huu kaulimbiu ya Kitaifa ni **“Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania.”**

Kaulimbiu hii inahimiza jamii ya watanzania kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na jitihada hizi lazima ziwe sehemu ya safari yetu ya maendeleo ya muda mrefu. Kukijanisha Tanzania kunamaanisha kulinda misitu yetu, kupanda miti kwa wingi, kutumia nishati safi ikiwemo nishati safi

ya kupikia, kusimamia rasilimali kwa uendelevu, na kupunguza uchafuzi wa mazingira.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Maadhimisho ya mwaka huu pamoja na mambo mengine yameambatana na shughuli mbalimbali ambazo ni pamoja na:

i. Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja na Mabadiliko ya Tabianchi;
ii. Ushiriki wa Viongozi na Wananchi katika shughuli za vielelezo za upandaji miti na usafi wa mazingira katika Majiji na Miji mbalimbali nchini ikiwemo *Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Tanga;*
iii. Upandaji Miti katika eneo la Mto Mkondoa, Wilaya ya Kilosa, Morogoro;
iv. Kongamano la Kisayansi na Utafiti wa Mazingira ambayo ni mojawapo ya shughuli za maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* pamoja na uzinduzi wa Kongamano la Wadau wa Mazingira *(Conference of Stakeholders on Environment (COSE),* Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNICC)*; Kongamano hili limehusisha washiriki takribani 100 kutoka ndani ya Nchi, na nchi jirani za afrika Mashariki.
v. Maadhimisho ya Miaka 40 ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNICC),* Dar es Salaam;
vi. Kongamano la Vijana kuhusu Hifadhi ya Mazingira, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM);
vii. Maonesho ya teknolojia na ubunifu kuhusu shughuli za uhifadhi wa mazingira, Viunga vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, Dodoma, Maonesho hayo yamekutanisha wadau kutoka Wizara,

Taasisi, Mashirika ya Umma, Taasisi Binafsi, Asasi za Kiraia, Vijana na Makundi mbalimbali. Aidha, maonesho haya yanatajiwa kuwa na mabanda takribani 100.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Na leo, ndio kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambapo hadhira hii iliopo hapa mbele yako pamoja na umma wa Watanzania unaotufuatilia mbashara kupitia vyombo vya habari unasubiria kwa hamkubwa kusikia nasaha zako na maelekezo yako kuhusu masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais, katika hafla hii tutakuomba utuzindulie Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Mazingira Kuelekea Dira 2050 itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026 – 2030). Programu hii inalenga kuchochea matokeo makubwa na ya haraka katika kurejesha uoto wa asili, kuimarisha ustawi wa mifumo ikolojia pamoja na huduma za kiikolojia ambazo ni msingi muhimu wa uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi. Hatua hizi zitachangia kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha malengo ya Dira ya 2050, ambayo inalenga kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi kumi (10) barani Afrika zenye ustawi wa mazingira na ustahimilivu mkubwa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Kupitia programu hii, Serikali inalenga kufanikisha malengo makubwa yafuatayo:

- Kuhamasisha upandaji na utunzaji endelevu wa miti bilioni mbili kila mwaka;
- Kurejesha hekta milioni tano za ardhi na misitu iliyoharibiwa;

- Kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa;
- Kuimarisha usimamizi wa taka na usafi wa mazingira;
- Kukuza biashara ya kaboni ili kuongeza mapato ya Taifa na kuchangia katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi; pamoja na
- Kuongeza ushiriki wa wananchi, hususan vijana na wanawake, katika shughuli za uchumi wa kijani na uhifadhi wa mazingira.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Maeneo ya kimkakati ya utekelezaji wa programu hii jumuishi ni Upandaji Miti katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, Geita, Singida, Simiyu, Manyara, Kilimanjaro, Dodoma na Rukwa, uanzishwaji wa Bustani za kijani katika maeneo ya miji; utunzaji na urejeshaji wa maeneo oevu ya Ziwa Natron, Bonde la Mto Mara, Bonde la Mto Malagarasi Myovosi na Bonde la Mto kilombero; kudhibiti viumbe vamizi katika maeneo ya mikoa ya Dodoma, Arusha, Mara, Mwanza na Manyara; usafi wa mazingira na urejelezaji wa taka ngumu katika majiji sita (6) na utekelezaji wa miradi 35 ya biashara ya kaboni katika sekta ya Usafirishaji, Misitu, Nishati na Usimamizi wa Taka.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Programu hii itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026–2030) kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za dini, washirika wa maendeleo pamoja na wananchi kwa ujumla. Mafanikio ya programu hii yatategemea zaidi ushiriki mpana wa jamii pamoja na uongozi thabiti katika ngazi zote.

Aidha, utekelezaji wake utaongeza fursa za ajira kwa vijana na wanawake, kuboresha uzalishaji katika sekta mbalimbali kama kilimo, mifugo na utalii,

pamoja na kuimarisha ustawi wa mifumo ikolojia ambayo ni msingi wa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Maandalizi ya programu hii yamezingatia uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mikakati iliyopita hapa nchini na katika nchi nyingine zinazotekeleza programu zinazofanana na hii. Utekelezaji wa programu hii unatarajiwa kugharimu takribani shilingi trilioni saba, ambazo zitatokana na Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia pamoja na washirika wa maendeleo.

Programu hii inahusia na Programu jumuishi ya kukijanisha Zanzibar inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanzia mwaka 2023 yenye lengo la kuimarisha ushirikiano miongoni mwa wadau wa mazingira; kujenga uhimilivu wa jamii dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Programu ya Zanzubar inahusisha upandaji, utunzaji, na uendelezaji wa miti kwa njia endelevu. Jumla ya miti 176,203 imepandwa katika jumla ya maeneo 35 yaliyopo Unguja (27) na Pemba (8) ambapo Unguja imepandwa miti 115,549 na Pemba miti 60,654 kwa kipindi cha mwaka 2024-2025 ikiwemo miti ya matunda, misitu, na mikoko.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Kwa kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa wadau katika maandalizi na utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo, pamoja na mchango wao katika utaalam na uwezeshaji wa rasilimali, Ofisi ya Makamu wa Rais ilishirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya Serikali katika maandalizi ya programu hii. Wadau hao ni pamoja na wizara za kisekta, sekta binafsi, washirika wa maendeleo pamoja na asasi za kiraia.

***Mheshimiwa Makamu wa Rais,***

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu kwa karibu utekelezaji wa programu hii kwa kushirikiana na wizara, taasisi za Serikali, mamlaka za serikali za mitaa pamoja na wadau wote ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

Kwa kutambua nafasi yako muhimu katika kuhamasisha Taifa na kuongoza juhudi za maendeleo endelevu, tunathamini sana uwepo wako katika tukio hili. Hakika, uzinduzi wa programu hii chini ya uongozi wako utaongeza msukumo na hamasa kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika kulinda na kuhifadhi mazingira yetu.

Baada ya maelezo hayo mafupi, napenda kuchukua fursa hii kukukaribisha Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ndiye Mgeni wetu rasmi ili uweze kutoa hotuba yako pamoja na kuzindua programu hii muhimu.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi naomba kuwasilisha!***